**UCHAMBUZI WA MUSWADA NAMBA 2 WA MWAKA 2026**

**Imewasilishwa;**

**Kamati ya Kudumu ya Bunge, Utawala, Katiba na Sheria**

**Tarehe 12 Agosti, 2026**

## A. Utangulizi

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimefanya uchambuzi na kuwasilisha maoni yake kuhusu *Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa mwaka 2026, uliochapishwa katika Gazeti Maalum la Serikali Na. 9, Juzuu ya 107 tarehe 5 Juni 2026.* Muswada unapendekeza marekebisho ya sheria kuu saba(7). Uchambuzi wa LHRC umejikita katika marekebisho ya sheria tatu (3) yanayogusa moja kwa moja haki za kumiliki mali, utawala wa kikatiba, uhuru wa mahakama na mamlaka ya taifa juu ya rasilimali asilia;

a) Marekebisho ya Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Sura ya 116).
b) Marekebisho ya Sheria ya Utajiri wa Asili na Rasilimali (Mamlaka ya Kudumu ya Taifa) (Sura ya 449).
c) Marekebisho ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori (Sura ya 283).

## B. Malengo

LHRC imefanya uchambuzi huu wa sheria ili kuhakikisha kuwa sheria zinazotungwa zinazingatia Haki za Binadamu, zinazingatia utawala wa sheria na utawala bora, zinalinda maslahi ya umma, na zinaendana kikamilifu na *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, pamoja na Mikataba ya Kimataifa na Kikanda ya Haki za Binadamu ambayo* Tanzania imeridhia.

## C. Tathmini ya Jumla na Mapendekezo

LHRC inapongeza hatua hii ya kuwasilisha hatua kadhaa za kisheria zenye mwelekeo chanya kupitia Muswada huu.

Kwa namna ya pekee, LHRC inakaribisha:

a) Kuondolewa kwa unyang'anyi wa lazima wa mifugo chini ya *Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori (Sura ya 283),* jambo linalokuza uwiano na usawa katika adhabu za jinai;
b) Kuwekwa kwa usawa kwa muda wa uongozi wa viongozi wa serikali za mitaa chini ya *Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) (Sura ya 287) na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) (Sura ya 288);*
c) Kuwekwa kwa muda maalum wa kisheria wa miaka mitatu kwa wajumbe wa Tume chini ya Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

Hata hivyo, LHRC imebaini mapungufu muhimu yanayohitaji hatua kutoka kwa Bunge, kama yanavyoelezwa hapa chini pamoja na mapendekezo ya LHRC;

### 1. SHERIA YA MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI, SURA YA 116

### a) Kutokuwepo kwa vigezo vya uteuzi vinavyotegemea sifa na uwezo

Kifungu cha 4 cha marekebisho yanayopendekezwa, pamoja na kuweka muda wa miaka mitatu (3) wa uongozi, hakijaweka wazi vigezo vya uteuzi vinavyotegemea sifa na uwezo kwa wajumbe wa Tume. LHRC inapendekeza Bunge liweke sharti la wazi la kisheria linalolazimisha kuwepo kwa vigezo vya uteuzi vilivyo wazi na vinavyotegemea sifa, uwezo ili kuhakikisha umahiri, uwajibikaji na uhuru wa kitaasisi.

### b) Tishio kwa majukumu ya msingi kutokana na mamlaka yasiyo na mipaka ya uwekezaji

Kifungu cha 5 kinapendekeza kuipa Tume mamlaka mapana ya kuwekeza fedha, jambo ambalo linaweza kuelekeza mgao mdogo wa bajeti ya umma kutoka kwenye majukumu yake ya msingi yasiyo ya kibiashara na hivyo kuhatarisha utekelezaji endelevu wa majukumu yake ya msingi ya kisheria.

LHRC inapendekeza Bunge liongeze kifungu kipya kinachoweka wazi kuwa uwekezaji ufanywe kwa fedha za ziada pekee, kwa kuzingatia kikamilifu matakwa ya *Sheria ya Fedha za Umma (Sura ya 348),* huku likihakikisha kuwa majuumu ya kisheria ya mipango ya matumizi ya ardhi yanapewa kipaumbele na kulindwa. Aidha, uwekezaji unaoweza kuathiri utekelezaji wa majukumu ya kisheria uzuiwe, na kuwe na sharti la kutoa taarifa za kila mwaka kuhusu uwekezaji kwa Waziri.

2. **SHERIA YA UTAJIRI WA ASILI NA RASILIMALI (MAMLAKA YA KUDUMU YA TAIFA), SURA YA 449**

a) **Kudhoofisha usimamizi wa Bunge juu ya mikataba ya uchimbaji na uendelezaji wa rasilimali**

Kuhamisha mamlaka ya kuidhinisha taratibu maalum za utatuzi wa migogoro kutoka Bungeni kwenda Baraza la Mawaziri kunapunguza kwa kiasi kikubwa uwazi, kwa kuwa mashauri na mijadala ya Baraza la Mawaziri hufanyika kwa usiri. Hali hii inakinzana moja kwa moja na *Vifungu vya 4 na 5 vya Sheria ya Utajiri wa Asili na Rasilimali (Mapitio na Majadiliano Upya ya Masharti Yasiyo ya Haki) (Sura ya 450) pamoja na Kifungu cha 16 cha Sheria ya Tasnia ya Uziduaji, 2015,* ambavyo vinaweka usimamizi wa rasilimali asilia chini ya Bunge.

b) **Kudhoofisha uhuru wa Mahakama na maendeleo ya sheria kupitia maamuzi ya ndani**

Kuzikwepa mahakama za ndani kunadhoofisha Ibara ya 107A ya Katiba, inayoweka utoaji wa haki chini ya uhuru wa Mahakama. Kuwapa wawekezaji wa kigeni misamaha ya kutumia mahakama za ndani kunaashiria kutokuamini mfumo wa mahakama wa Tanzania na kunanyima nafasi ya maendeleo ya sheria na jurisprudence ya ndani.

Mifano ya kikanda, ikiwemo *Sheria ya Ulinzi wa Uwekezaji ya Afrika Kusini (2015)* na *Sheria ya Madini ya Kenya (2016),* inaweka kipaumbele katika mifumo ya ndani ya utatuzi wa migogoro ili kulinda mamlaka ya kitaifa ya udhibiti.

LHRC inapendekeza Bunge liimarishe Kifungu cha 11(4) kinachopendekezwa kwa kubadilisha idhini ya Baraza la Mawaziri na kuweka idhini ya Bunge kwa

makubaliano yoyote yanayotoa utaratibu maalum wa utatuzi wa migogoro. Aidha, kuwe na sharti la lazima la kumaliza kwanza njia zote za kisheria katika mahakama za ndani kabla ya kupeleka mgogoro kwenye mifumo ya kimataifa ya utatuzi wa migogoro. Sambamba na hilo, Serikali inapaswa kuwekeza katika kuimarisha ufanisi na uaminifu wa **mfumo wa mahakama za ndani nchini Tanzania ili kuongeza imani kwa wawekezaji na wananchi kwa ujumla.**

### 3. SHERIA YA UHIFADHI WA WANYAMAPORI, SURA YA 283

### a) Kutokuwepo kwa ulinganifu wa sheria za uhifadhi

**Vifungu vya 25 na 26** vya marekebisho yanayopendekezwa vinakusudia kuondoa unyang'anyi wa moja kwa moja wa mifugo chini ya Sura ya 283, kwa lengo la kulinda jamii za wafugaji zinazoishi pembezoni mwa hifadhi za wanyamapori. Hata hivyo, kuacha sheria nyingine zinazohusiana, kama vile *Sheria ya Hifadhi za Taifa (Sura ya 282) na Sheria ya Misitu (Sura ya 323),* bila marekebisho kunasababisha kuwepo kwa mfumo wa sheria wenye viwango viwili na wa kibaguzi.

Wafugaji wanaoishi pembezoni mwa Hifadhi za Taifa bado wataendelea kukabiliwa na unyang'anyi wa moja kwa moja wa mifugo kwa vitendo vinavyofanana, jambo linalokiuka haki ya ulinzi sawa chini ya *Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.*

LHRC inapendekeza kufanyika kwa wakati huo huo kwa marekebisho ya *Sheria ya Hifadhi za Taifa (Sura ya 282) na Sheria ya Misitu (Sura ya 323)* ili kuoanisha mfumo wa kisheria, kufafanua wazi hadhi ya kisheria ya mifugo inayozurura au kuingia katika maeneo yaliyohifadhiwa, na kupiga marufuku unyang'anyi wa moja kwa moja wa mifugo katika aina zote za maeneo yaliyohifadhiwa.

**WITO WA LHRC**

LHRC inatoa wito Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Muswada wa Marekebisho ya *Sheria ya Uthamini na Wathamini Sura Namba 138* katika hali yake ya sasa, na badala yake kupitisha mtazamo mpana na shirikishi katika kufanya marekebisho ya sheria hiyo.

LHRC inasisitiza kuwa Kifungu cha 70 cha Sheria kinampa Waziri mamlaka mapana ya kutunga kanuni kuhusu masuala mbalimbali bila kuweka misingi na miongozo ya wazi ya kuhakikisha maslahi ya wananchi na Serikali yanalindwa.

**Kwa mfano, Kanuni ya 64(1)(e)(x) ya Tangazo la Serikali Na. 136 la mwaka 2018 inamtaka mthamini kujaza Fomu ya Uthamini Na. 4,** ambayo inaonesha thamani ya mali zinazohusika katika mchakato wa fidia. Hata hivyo, mfumo wa kanuni uliopo hauhitaji nakala ya **Fomu Na. 4** iliyojazwa kukabidhiwa kwa mtu aliyeathirika ili aweze kuithibitisha na kukagua usahihi wa taarifa zilizorekodiwa, pamoja na kuhakikisha kuwa maendeleo na maboresho yote yaliyofanywa kwenye mali hiyo yameainishwa ipasavyo.

Pengo hili linaibua masuala ya msingi kuhusu uwazi, haki ya kufuata taratibu stahiki, na ulinzi wa haki za watu wanaoathiriwa na michakato ya uthamini na ulipaji wa fidia.

**Imetolewa na;**

**Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)**

Kwa maelezo zaidi pakua uchambuzi kamili kwenye tovuti www.humanrights.or.tz